KWAYA YA MTAKATIFU KIZITO
PAROKIA YA MWENYEHERI ANUARITE MAKUBURI
+255742000089|+255713975788
kmkmakuburi
www.kmkmakuburi.co.tz
stkizitochoir@gmail.com

UPOKEE BABA, SADAKA TUNAYOTOA-J. MAKOYE

Kiitikio

Upokee Baba, (upokee) sadaka tunayotoa, ni sadaka yake mwanao Mpenzi

Mashairi

1. Ni sadaka ya kweli, isiyo na doa, ni sadaka yake, mfalme wetu
2. Kageuza mkate kuwa mwili wake, kwa mapendo yake tupate kula
3. Kageuza divai kuwa damu yake, kwa mapendo yake tupate kunywa
4. Alijinyenyekeza hata msalabani, kifo akapata ili tuishi
5. Utukufu wa Yesu unadhihirika, yeye ndiye mfalme wa ulimwengu